HISTORIA YA PAROKIA YA MT. POLYCARP MISUGUSUGU

Ukatoliki katika eneo la Misugusugu ulianza na familia tano (5) mwaka 1971 zikiongozwa na Marehemu Mzee Nemes Daudi Luzua aliyehamia katika Kijiji cha Misugusugu kutoka Matombo Morogoro. Mzee Nemes aliungana na familia za Marehemu Mzee Athanas Masenga aliyehamia toka Parokia ya Lugoba, pamoja na familia za Marehemu Mzee Arbogast Matembele, Amandus Mponda, na Gustav Mtumbuka aliyehamia Misugusugu akitokea Kipatimu.

Familia hizi tano zilikuwa zikikutana nyumbani kwa Mzee Nemes kwa sala chini ya mti wa mkorosho tangu mwaka 1971. Wakati huo hapakuwepo Kigango wala Jumuiya. Watu wengi katika familia hizi hawakuwa wamebatizwa wala kufunga ndoa.

Mwaka 1972 Katekista wa kwanza aliyetembelea familia hizi alikuwa Fabian Mwageni, akitokea Kigango cha Kibondeni Parokia ya Tumbi, kwa sasa Parokia ya Mkuza. Katekista Fabian Mwageni alishirikiana na Mzee Nemes Daudi kutoa mafundisho ya Ukatekumeni kwa familia hizi kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo hadi mwaka 1973, ambapo Katekista Fabian alihamishwa na badala yake akaletwa Katekista Thadei Kunambi. Mwaka 1974 Katekista Kunambi alikamilisha mafundisho na Sakramenti za Ubatizo, Kitubio, Ekaristi, Kipaimara na Ndoa zilitolewa. Kulikuwa na Ndoa tatu mwaka huo: Athanas Masenga na Anna Mwanga; Arbogast Matembele na Sofina Mwanga; na Amandus Mponda na Hendrika Kisome. Huduma hii ya Masakramenti ilitolewa na Padre Meinhard Inauen (Mkapuchini) aliyekuwa Paroko wa Kibaha/Tumbi wakati huo.

Mwaka 1976 idadi ya waumini iliongezeka kidogo ikabidi kuomba kutumia chumba cha darasa katika Shule ya Msingi Misugusugu kwa ajili ya ibada ya Misa siku za Jumapili. Siku za Jumapili alikuwa akifika paroko msaidizi Padre Emilian ambaye aliwashauri waamini kutafuta eneo la kujenga Kanisa. Mzee Nemes alitoa eneo lakini lilionekana kuwa na maji kipindi chote cha mwaka. Paliachwa kwa ajili ya kuzikia waamini marehemu wakatoliki. Lilipatikana eneo lingine katika kitongoji cha Vitendo kwenye mashimo ya mchanga ambapo kulionekana kuwa mashimo ni mengi mno na hapakuwa na waumini walio karibu. Mwisho Marehemu Mzee Matembele alitoa eneo la robo ekari ambalo liliafikiwa na Padre Emilian kwa kuwa na familia nyingi za kikatoliki karibu na eneo hilo. Mwaka 1979 ujenzi wa jengo la ibada ulifanyika.

Mwaka 1980 Misugusugu ilitangazwa kuwa Kigango rasmi chini ya Parokia ya Tumbi/Kibaha. Katekista na Mwenyekiti wa kwanza wa Kigango alikuwa Mzee Nemes Daudi. Baadaye ilionekana ni vyema Mzee Nemes apate msaidizi kutokana na umri wake; hivyo Patrick Matembele aliteuliwa kwenda kupata kozi fupi ya ukatekista. Aliporudi aliendelea na kazi ya ukatekista kwa kipindi cha mwaka mmoja halafu akaacha kazi hiyo. Kigango kiliendelea kupata huduma toka parokia ya Tumbi chini ya mapadri wafuatao kwa vipindi tofauti: Padre Maseko, Padre Mbiku na Padre Venence Tegete.

Mwaka 1984 Padre John Laane (Maryknoll) alikuwa Paroko wa Kibaha/Tumbi. Mwaka 1985 idadi ya waumini ikawa imeongezeka na changamoto mbalimbali zikawa zimejitokeza na hivyo ikaamuliwa kuwa waumini watumie tena chumba cha darasa katika shule ya msingi Misugusugu kwa ajili ya ibada badala ya jengo lililojengwa kwa Mzee Arbogast Matembele. Wakati ibada ikiendelea kufanyika shuleni kiwanja cha ukubwa wa robo ekari kilipatikana kandokando ya barabara ya Morogoro mkabala na shule ya msingi.

Mwaka 1986 uongozi wa Kigango ukawa chini ya Mwenyekiti Gustav Mtumbuka na Katekista Nemes Daudi akisaidiwa na kijana Elias Masenga. Mwaka 1987 kijana Elias Masenga alichaguliwa na Halmashauri ya Kigango na kuthibitishwa na Paroko John Laane kuwa Katekista wa Kigango.

Mwaka 1989 Kigango kilipata jengo la pili la ibada la muda lililojengwa kwenye kiwanja pembezoni mwa barabara ya Morogoro chini ya uongozi wa Nd. James Temu kama Mwenyekiti.

Mwaka 1995 Kigango cha Mlandizi kilipandishwa hadhi na kuwa Parokia ya Mt. Anthony wa Padua, na hivyo Kigango cha Misugusugu kilihamishwa toka usimamizi wa Parokia ya Tumbi kuwa chini ya Parokia ya Mlandizi ikiongozwa na Paroko wake wa kwanza Padre Joseph Kanduta. Kigango cha Misugusugu kiliendelea kupata huduma katika jengo lake lililokuwa karibu na barabara kutoka kwa mapdri wa parokia ya Mlandizi wakisaidiwa na mapadri waliokuwa wakifundisha katika Seminari ndogo ya Mt. Maria Visiga. Ilipofika mwaka 2008 idadi ya waamini iliongozeka kiasi cha uhitaji wa eneo kubwa na jengo la kudumu kupewa kipaumbele.

Baada ya kuona kuwa ni gharama sana kupata eneo lingine kutokana na uhaba wa pesa, lilipatikana wazo la kubadilisha eneo la robo ekari lililokuwa likitumika wakati huo kwa eneo la ekari mbili toka kwa Mzee John Maganga. Baada ya makubaliano kukamilika na mikataba kusainiwa ujenzi wa banda la muda la ibada lilijengwa. Kwa hiyo Kigango kilihamia katika eneo la hekari mbili mwaka 2009 pakiwa na idadi ya Jumuiya sita. Huduma ilianza kutolewa katika hilo banda la muda wakati huo huo harakati kabambe za ujenzi wa nyumba ya Katekista ukiendelea, kwa kuwa wakati huo huduma za katekesi zilitolewa na makatekista wawili wa kujitolea walikuwa ni miongoni mwa waamini (Elias Masenga na Gasper Ndakidemi). Nyumba ya Katekista ilipokamilika aliajiriwa Katekista aliyefuzu mafunzo ya Katekesi/ukatekista. Baada ya kukamilisha nyumba na ajira ya Katekista, ujenzi wa jengo la kudumu la ibada ulianza mwishoni mwa mwaka 2010, pakiwa na idadi ya Jumuiya 10. Ujenzi ulichukuwa takribani miaka miwili na ilipofika Desemba 2012 Jengo lilikamilika na kubarikiwa tarehe 27 Desemba 2012 na Monsinyori Deogratias Mbiku.

Baada ya jengo la kudumu kukamilika na kubarikiwa mchakato wa kuanza ujenzi wa nyumba ya mapadri ulianza. Katikati ya mwaka 2013 Mwadhama Kardinali alitembelea Kigango na

kutushauri tusijenge nyumba ya mapadri bali tujitahidi tuongeze eneo la kutosha maana ekari mbili kwa parokia hazitoshi. Hivyo, ndoto za ujenzi wa nyumba ya mapadri uliyeyuka na hapo hapo mchakato wa kuongeza eneo ulianza. Baada ya kukutana na vikwazo vizito katika harakati za kupata eneo, maombi ya dhati yalipelekwa kwa Yesu wa Ekaristi. Muujiza wa Ekaristi Takatifu ulifanyika na tukapata ekari tatu na kufanya eneo letu kuwa na ekari tano. Baada ya kuongeza eneo mchakato wa ujenzi wa nyumba ya mapadri ulianza tena. Wakati mchakato wa ujenzi ukiendelea iliongezwa ekari moja baada ya jirani kuonyesha azma ya kuuza tena ekari moja. Hivyo eneo la Kigango likawa na ukubwa wa ekari sita.

Ilipofika Julai 2016 ujenzi wa nyumba ya mapadri ulianza na kukamilika Juni 2017. Kwa neema na Baraka zake Mwenyezi Mungu, Baba Mwadhama alitangaza Kigango cha Misugusugu kuwa Parokia ya Mt. Polycarp siku ya tarehe 7 Julai 2017. Shauku na hamu kubwa ya waamini wa Misugusugu ya kupata Misa Takatifu kila siku ilifikia upeo. Safari za kila siku asubuhi kwenda Visiga Seminari kwa ibada ya Misa ziliisha na kupata huduma hiyo kwa karibu. Tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa mema mengi aliyotujalia. Mungu amjalie Mwadhama Kardinali Pengo afya njema kwa upendo wake kwa waamini wa Misugusugu. Vigango vya ZOGOWALE, NGETA NA MAKAZI MAPYA vimewekwa chini ya parokia ya Mt. Polycarp Misugusugu. Kwa hiyo, Parokia kwa sasa ina Vigango 3 na Kanda 2; vyote vikiwa na Jumuiya 22.

Maandalizi ya uzinduzi wa Parokia yetu umeleta neema hizi:

- Watoto 130 wamebatizwa
- Ndoa 27 zimebarikiwa
- Mapadre wetu wamefanikiwa kutembelea familia zote nyumba kwa nyumba kuwafahamu waumini na kuamsha uhai wa imani.

MIPANGO YA BAADAYE

1. Kuongeza eneo letu kufikia ekari 8
2. Kuanzisha vituo vya sala sehemu zenye waamini zilizo mbali na parokia
3. Kusaidia Vigango vya Zogowale, Makazi Mapya na Ngeta kukamilisha majengo ya ibada
4. Kujenga ofisi za Parokia
5. Kujenga Kanisa Kubwa la Kudumu Parokiani
6. Kujenga Zahanati/Kituo cha Afya
7. Kujenga nyumba ya Masista
8. Kujenga shule ya awali katika eneo parokia lililopo barabarani
9. Kujenga chuo cha ufundi

TUMSHUKURU MUNGU KWA MEMA YOTE ANAYOTUJALIA